BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2019

## 06 URAIA NA MAADILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2019

# 06 URAIA NA MAADILI

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019**

Haki zote zimehifadhiwa.

**YALIYOMO**

DIBAJI ........................................................................................................iv

1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1

2.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WANAFUNZI KWA KILA SWALI 2

2.1 Sehemu A (Alama 26) ...................................................................2

2.2 Sehemu B (Alama 24) .................................................................17

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI………………………………………………....27

4.0 HITIMISHO .......................................................................................... 28

5.0 MAPENDEKEZO ................................................................................. 28

KIAMBATISHO A .................................................................................... 29

KIAMBATISHO B .................................................................................... 30

# DIBAJI

Taarifa hii ni ya Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Uraia na Maadili 2019. Imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera na wadau wengine wa elimu kuhusu maarifa, stadi na mielekeo ambayo wanafunzi waliweza kupata au kutopata katika kipindi cha miaka minne ya Elimu ya Msingi. Mtihani wa Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa mwaka 2019 katika somo hili ulitayarishwa kwa kuzingatia mabadiliko ya Mtaala wa Elimu ya Msingi kwa Darasa la III hadi IV wa mwaka 2016. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika upimaji huu unaweza kutumika kama kipimo cha ufanisi katika utekelezaji wa mtaala huo kwa lengo la kuboresha utoaji wa elimu inayowajengea wanafunzi uwezo katika umahiri mbalimbali kwa somo la Uraia na Maadili.

Katika taarifa hii, mambo yaliyochangia ufaulu wa wanafunzi kwa kila swali yameainishwa. Taarifa inaonesha kuwa, wanafunzi waliofanya vizuri walielewa vema matakwa ya swali na walikuwa na maarifa ya kutosha katika umahiri uliopimwa. Wale ambao hawakufanya vizuri, ama walishindwa kutambua matakwa ya swali, walikuwa na uelewa mdogo wa umahiri mbalimbali uliopimwa, au hawakuwa na Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Mwisho wa taarifa hii kumewekwa kiambatisho kinachoonesha jinsi wanafunzi walivyofaulu katika kila umahiri uliopimwa.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa mamlaka husika zitahakikisha kuwa dosari zilizoainishwa

katika taarifa hii zinapatiwa ufumbuzi ili kuongeza ujuzi na maarifa ya wanafunzi.

Mwisho, Baraza linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Uraia na Maadili ulifanyika tarehe **20** mwezi Novemba mwaka 2019. Upimaji huu ulizingatia muhtasari wa mwaka 2016 ambao umelenga katika kuwajengea wanafunzi umahiri ambao ulipimwa kupitia utendaji wa wanafunzi katika kubaini maarifa, stadi na mwelekeo walionao katika kufikia umahiri mahsusi ulioainishwa. Hivyo, viwango vya utendaji wa wanafunzi katika upimaji huo viligawanyika katika makundi manne; Kiwango hafifu, Kiwango cha wastani, Kiwango kizuri na Kiwango kizuri sana. Wanafunzi waliokuwa na utendaji hafifu walihesabika kufeli na wanafunzi waliokuwa na utendaji wa wastani hadi utendaji mzuri sana walihesabika kufaulu upimaji huo.

Jumla ya wanafunzi 1,786,729 walijiandikisha kufanya upimaji ambapo wanafunzi 1,663,803 walifanya upimaji huu. Aidha, ufaulu wa wanafunzi katika somo hili unaonesha kuwa wanafunzi 1,584,685 sawa na asilimia 95.26 walifaulu, na wanafunzi 78,853 sawa na asilimia 4.74 hawakufaulu. Ufaulu huu umepanda ikilinganishwa na mwaka 2018 ambapo wanafunzi 1,207,664 (92.8%) walifaulu na wanafunzi 93,660 (7.2%) hawakufaulu.

Upimaji ulikuwa na jumla ya maswali sita (6) yenye jumla ya vipengele 25, vilivyogawanyika katika sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali matatu (3) yenye jumla ya vipengele 13 ambavyo vilikuwa na jumla ya alama 26. Sehemu B ilikuwa na maswali matatu (3) yenye jumla ya vipengele 12 ambavyo vilikuwa na jumla ya alama 24. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kutoka sehemu zote A na B. Upimaji ulikuwa na jumla ya alama 50.

Katika sehemu A kulikuwa na maswali ya kuchagua ambapo wanafunzi walitakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuandika katika kisanduku, kuoanisha maelezo kuhusu alama za taifa yaliyoainishwa katika fungu A na alama za taifa katika fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi, na kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi. Aidha, katika sehemu B wanafunzi walitakiwa kuweka alama ya vema kuonesha kama zana zilizooneshwa katika jedwali ni za asili au siyo za asili, kuchunguza picha, kisha kujibu maswali, na kusoma kwa umakini kifungu cha habari, na kisha kujibu maswali.

Taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya upimaji wa somo la Uraia na Maadili itajikita kuangalia maswali yote sita yaliyotoka katika umahiri

mbalimbali ulioainishwa katika muhtasari. Uchambuzi huu, pia unabainisha idadi au asilimia ya wanafunzi walioweza au walioshindwa kuchagua jibu sahihi na kueleza sababu zilizofanya wachague majibu hayo.


Viwango vya kufaulu kwa kila swali vimezingatia asilimia ya wanafunzi waliofaulu katika swali husika. Iwapo asilimia 0 - 33 ya wanafunzi waliweza kujibu swali hilo vizuri, kiwango cha kufaulu kwa swali hilo kilihesabika kuwa ni hafifu. Kwa upande mwingine kama wanafunzi walioweza kufanya swali hilo vizuri ni kati ya asilimia 34 – 66, kufaulu katika swali hilo kulihesabika kuwa ni kwa wastani. Kiwango cha kufaulu kilihesabika kuwa ni kizuri iwapo watahiniwa walioweza kufanya swali hilo vizuri ni kati ya asilimia 67 – 100. Aidha, chati za viwango vya kufaulu zimeambatishwa ili kufafanua kufaulu kwa wanafunzi ambapo rangi ya kijani inawakilisha kufaulu kwa kiwango kizuri, rangi ya njano inawakilisha kufaulu kwa kiwango cha wastani na kufaulu kwa kiwango hafifu kunawakilishwa na rangi nyekundu.

## 2.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WANAFUNZI KWA KILA SWALI

### 2.1 Sehemu A (Alama 26)

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu ambapo swali la 1 lilikuwa la kuchagua herufi ya jibu sahihi lenye jumla ya alama 10. Swali la 2 lilikuwa la kuoanisha lenye jumla ya alama 8. Swali la 3 lilikuwa la kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi na lilikuwa na jumla ya alama 8. Jumla ya alama katika sehemu hii ni 26. Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika sehemu hii.

**Swali la 1:** Swali hili lilikuwa na vipengele vitano vya maswali ya kuchagua jibu sahihi vilivyotoka katika umahiri *Kuwa mstahimilivu*. Kila kipengele kwenye swali hili kilikuwa na jumla ya alama 2. Jumla ya wanafunzi 1,663,778 walifanya swali hili ambapo wanafunzi 130,378 (7.8%) walifanya vizuri sana kwa kupata alama zote 10; wanafunzi 355,245 (21.4%) walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu kwa kupata alama 8; wanafunzi 838,244 (50.4%) walikuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu kwa kupata alama 4 hadi 6, na wanafunzi 339,911 (20.4%) walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata alama 0 au 2 kama inavyoonekana katika Chati Na. 1.




**Chati Na. 1**: *Kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali la 1.*

Chati Na. 1 inaonesha kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili kulikuwa kwa kiwango kizuri kwa kuwa asilimia 79.6 ya wanafunzi waliweza kupata kuanzia alama 4 hadi 10.

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele.

(i) Unapaswa kufanya nini unapoishi na watu wenye tabia zisizokubalika katika jamii?

A Kuwakimbia bila kuwashauri

B Kuwavumilia na kuwashauri

C Kupigana nao hadi wabadilike

D Kuwatolea maneno makali

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kuvumilia katika Maisha ya Kila Siku.* Kililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kujenga tabia ya kuwakubali watu wengine kulingana na tabia zao jinsi zilivyo. Wanafunzi walioweza kubaini jibu sahihi B, *Kuwavumilia na kuwashauri* walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya tabia za watu wenye tabia zisizokubalika katika jamii. Aidha, walikuwa na uelewa wa njia za kuishi na watu wenye tabia zisizokubalika katika jamii wanazoishi, kama vile kupigana na wengine, kuiba, kutoa maneno mabaya, kucheka wengine, kutokubali wengine, n.k.

Wanafunzi hao walikuwa na maarifa kuwa watu wenye tabia zisizokubailika katika jamii zao wanahitaji kuvumiliwa na kupewa ushauri na si kuwakimbia.

Wanafunzi walioshindwa kubaini jibu sahihi kwa kuchagua vipotoshi A, *Kuwakimbia bila kuwashauri*, C, *Kupigana nao hadi wabadilike* na D, *Kuwatolea maneno makali* hawakuwa na uelewa kuhusu njia za kuchukua katika kuishi na watu wenye tabia zisizokubalika katika jamii. Wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Kuwakimbia bila kuwashauri* walitumia ushauri wanaoupata mara kwa mara kutoka kwa wazazi kuhusu kuepuka kuwa na marafiki wenye tabia mbaya.

Aidha, wanafunzi waliochagua vipotoshi C, *Kupigana nao hadi wabadilike* na D, *Kuwatolea maneno makali* walihusianisha na hatua ambazo huchukuliwa kwa watu wenye tabia zisizokubalika katika jamii zao, kwa mfano watu wanavyo jichukulia sheria mkononi kwa kuwapiga wezi na kuwachoma moto. Vilevile, katika ngazi ya familia wazazi walio wengi huwaadhibu watoto wao ambao wana tabia zisizokubalika kwa kuwatolea maneno makali na kuwapiga.

(ii) Njia ipi inaweza kutumika katika kutatua changamoto zinazokukabili?

A Kuzikubali na kuweka malengo

B Kuwa ombaomba na kutaka ushauri

C Kuchoka na kukata tamaa

D Kuweka malengo na kuyaacha

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kufikia malengo uliyojiwekea kwa kuwa na mtazamo chanya.* Kililenga kupima uwezo wa wanafunzi katika kutambua njia wanazoweza kutumia katika kutatua changamoto wanazokutana nazo katika maisha ya kila siku kwenye jamii husika. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi A, *Kuzikubali na kuweka malengo* walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu njia ambazo mtu anaweza kutumia katika kutatua changamoto zinazomkabili. Wanafunzi hao walielewa kuwa unapoikubali changamoto unajenga uwezo wa kuikabili na unatakiwa kuwa makini ili kupata ufumbuzi kwa kuweka malengo.

Wanafunzi walioshindwa kubaini jibu sahihi kwa kuchagua vipotoshi B, *Kuwa ombaomba na kutaka ushauri,* C, *Kuchoka na kukata tamaa* na D, *Kuweka malengo na kuyaacha* hawakuwa na uelewa juu ya njia sahihi inayoweza kutumika katika kutatua changamoto zinazokukabili. Wanafunzi waliochagua kipotoshi B, *Kuwa ombaomba na kutaka ushauri* walihusisha tabia ya watu kuomba msaada na ushauri wanapopata changamoto. Hata hivyo, walishindwa kutambua kuwa kuomba msaada sio kuwa ombaomba wakati tabia ya kuwa ombaomba ni tabia mbaya ya kutopenda kujishughulisha. Wanafunzi waliochagua vipotoshi C, *Kuchoka na kukata tamaa* na D, *Kuweka malengo na kuyaacha* walishindwa kutambua kuwa hizo ni tabia ambazo huoneshwa na watu wanaokata tamaa mapema katika kutatua changamoto zinazowakabili katika maisha yao. Tabia hizo husababisha watu kujiingiza kwenye vitendo vibaya, kama vile kuiba, kuwa ombaomba, kujihusisha katika ngono za utotoni au kujidhuru wenyewe kwa kukosa suluhisho.

(iii) Lipi kati ya matendo yafuatayo yanaonesha tabia ya ustahimilivu?

A Kudadisi bila kuchoka na kupata jibu

B Kufanya kazi kwa bidii na kupumzika sana

C Kufanya kazi haraka haraka

D Kufanya kazi polepole

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kuvumilia katika maisha ya kila siku.* Kipengele kiliwataka wanafunzi kufahamu matendo yanayoonesha tabia ya ustahimilivu wa mtu katika maisha ya kila siku. Wanafunzi waliopata jibu sahihi A, *Kudadisi bila kuchoka na kupata jibu* walikuwa na uelewa kuhusu matendo yanayoonesha tabia ya ustahimilivu. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa kwamba katika maisha ya kila siku watu wanapaswa kuwavumilia wengine wenye tabia tofauti na zao, na pia wanatakiwa kustahimili matatizo na changamoto zinazowakabili ili kupata suluhisho.

Wanafunzi waliochagua kipotoshi B, *Kufanya kazi kwa bidii na kupumzika sana* walijibu kwa mazoea kutoka kwenye jamii zao ya kuwa baada ya kazi ngumu mtu hutakiwa kupumzika. Wanafunzi hao walishindwa kubaini kupumzika sana huondoa uhalisia wa kufanya kazi kwa bidii na si miongoni mwa matendo ya mtu mstahimilivu.

Aidha, wanafunzi waliochagua kipotoshi C, *Kufanya kazi harakaharaka* na D, *Kufanya kazi polepole* hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya matendo yanayoonesha tabia ya ustahimilivu. Wanafunzi waliochagua *Kufanya kazi harakaharaka* walijua kwa kufanya kazi harakaharaka unaweza kumaliza kwa wakati na walishindwa kutambua ya kuwa tendo hilo si miongoni mwa matendo yanoyoonesha tabia ya mtu kuwa mstahimilivu. Waliovutiwa na kipotoshi *Kufanya kazi polepole* huenda walihusianisha na methali maarufu ya kiswahili "*haraka haraka haina Baraka"*. Hivyo, wanafunzi hao waliamini kufanya kazi polepole ni miongoni mwa matendo ya ustahimilivu.

(iv) Kuhimili vikwazo katika maisha kunatuwezesha kufikia __________.

A matatizo yetu ya kila siku.

B heshima yetu.

C ugumu wa maisha.

D malengo yetu.

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kuvumilia katika maisha ya kila siku* na kililenga kubaini uwezo wa mwanafunzi kubaini matokeo/faida ya kuhimili vikwazo katika maisha ikiwa ni pamoja na kumwezesha mtu kufikia malengo yake. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi D, *Malengo yetu* ni dhahiri walikuwa na uelewa kuhusu faida ya kuhimili vikwazo katika maisha ya kila siku. Wanafunzi hao walitambua kuwa kitendo cha kuhimli vikwazo katika maisha ya kila siku kinaweza kumfanya mtu kufikia malengo aliyojiwekea, kama vile kufaulu mitihani yao au kukamilisha kazi fulani kwa wakati.

Wanafunzi wachache walivutiwa na vipotoshi A, *Matatizo yetu ya kila siku*, B, *Heshima yetu* na C, *Ugumu wa maisha*. Wanafunzi waliochagua kipotoshi B, *Heshima yetu* walishindwa kuelewa kuwa mtu anaweza kupata heshima baada ya kufanya jambo fulani lakini asifikie malengo yake. Hawakuwa na uelewa kuwa katika jamii watu uhimili vikwazo mbalimbali kwa sababu ya kufikia malengo yao waliyojiwekea, kwa mfano kutembea umbali mrefu kuazima vitabu vya kujisomea ili kufaulu mitihani.

Aidha, wanafunzi waliochagua vipotoshi A, *Matatizo yetu ya kila siku* na C, *Ugumu wa maisha* walishindwa kutambua kwamba matatizo ya kila siku na ugumu wa maisha ni sehemu ya vikwazo ambavyo mtu anatakiwa

kuvihimili ili kufikia malengo yake na si matokeo/faida ya kuhimili vikwazo katika maisha.

(v) Hali ya kujiamini na kutarajia mafanikio katika jambo fulani hujulikana kama ________________________.

A Udadisi.

B Changamoto.

C Mtazamo chanya.

D Uvumilivu.

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kufikia malengo uliyojiwekea kwa kuwa na mtazamo chanya.* Kilipima uwezo wa wanafunzi katika kubaini matendo yenye kuonesha mtazamo chanya. Wanafunzi walioweza kubaini jibu sahihi C, *Mtazamo chanya* walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu tabia ya mtazamo chanya na walifahamu vema faida za kuwa na mtazamo chanya katika kukamilisha kazi yenye mafanikio. Wanafunzi hao walitambua kuwa hali ya kujiamini na kutarajia mafanikio katika jambo fulani na kuwa na imani ya kwamba unaweza kufanikiwa katika jambo fulani ni mtazamo chanya.


Wanafunzi walioshindwa kubaini jibu sahihi kwa kuchagua vipotoshi A, *Udadisi*, B, *Changamoto* na D, *Uvumilivu* hawakuwa na ufahamu juu ya tabia zinazoonesha mtazamo chanya. Wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Udadisi* walichanganya vitendo vya udadisi na mtazamo chanya kwa kuwa katika kufikia mafanikio, udadisi wa mambo unahitajika ili kupata ukweli wa jambo fulani. Walishindwa kutambua kuwa udadisi pekee hautoshi kuwa ni tabia ya mtazamo chanya.

Wanafunzi waliochagua vipotoshi B, *Changamoto* na D, *Uvumilivu* waliamini kuwa ili ufikie malengo lazima upitie changamoto mbalimbali na lazima uwe mvumilivu. Wanafunzi hawa walishindwa kutambua maana halisi ya maneno hayo. Changamoto ni mambo ambayo yanaweza kusababisha jambo fulani lisifanikiwe na uvumilivu ni hali ya kuhimili katika shida, tabu au changamoto fulani.

**Swali la 2:** Jibu kipengele (i) - (iv) kwa kuoanisha maelezo kuhusu alama za Taifa katika **Fungu A** na alama za Taifa katika **Fungu B**. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

<table>
<tr><th colspan="2">Fungu A</th><th>Herufi</th><th>Fungu B</th></tr>
<tr><td>(i)</td><td>Huonesha utajiri wa mali asili ya nchi yetu.</td><td>( )</td><td rowspan="4">A. Bendera ya taifa<br>B. Jembe na nyundo<br>C. Wimbo wa taifa<br>D. Nembo ya taifa.<br>E.Fedha za Tanzania<br>F. Pembe za ndovu</td></tr>
<tr><td>(ii)</td><td>Hutumika katika barua za kiofisi na machapisho ya serikali.</td><td>( )</td></tr>
<tr><td>(iii)</td><td>Huashiria uhuru wa nchi yetu.</td><td>( )</td></tr>
<tr><td>(iv)</td><td>Huwakilisha vifaa vinavyotumika kuendeleza taifa.</td><td>( )</td></tr>
</table>

Swali hili lilikuwa na vipengele vinne vilitoka katika Umahiri mkuu *Kuwa mwajibikaji* na kwenye umahiri mahususi *Kulinda rasilimali na maslahi ya nchi.* Swali hili lililenga kupima uwezo wa wanafunzi katika kubaini maana za alama mbalimbali za taifa. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani ni asilimia 44 tu ya wanafunzi 1,663,778 ndio walipata kuanzia alama 4 hadi 8, wakati asilimia 56 walishindwa kwa kupata alama 0 au 2. **Chati Na. 2** inaonesha takwimu za ufaulu katika swali la 2.




**Chati Na. 2**: *Kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali la 2.*

Chati Na. 2 inaonesha kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili kulikuwa kwa kiwango cha wastani kwa kuwa asilimia 44 ya wanafunzi wote waliofanya swali hili walipata daraja A hadi D.

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele.

Kipengele cha (i) kilipima uwezo wa wanafunzi katika kubaini alama ya taifa inayoonesha utajiri wa mali asili ya nchi yetu. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi F, *Pembe za ndovu* walikuwa na uelewa sahihi kuhusu maana ya *pembe za ndovu*, hivyo walitambua kuwa alama hiyo huonesha utajiri wa mali asili ya nchi yetu. Wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Bendera ya taifa* hawakuelewa kuwa Bendera ya Taifa huashiria uhuru wa nchi yetu na si kuonesha utajiri wa mali asili ya nchi yetu. Wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi B, *Jembe na nyundo* walishindwa kutambua kuwa *jembe na nyundo* huwakilisha vifaa vinavyotumika kuendeleza taifa. Aidha, wanafunzi wengi walivutiwa na kipotoshi C, *Wimbo wa Taifa* kwa kuwa beti ya pili na tatu ya wimbo wa taifa huzungumzia uzuri na baraka za nchi yetu, hivyo walihusisha na utajiri wa mali asili ya nchi yetu. Wanafunzi waliochagua kipotoshi D, *Nembo ya Taifa* walishindwa kutambua kuwa *Nembo ya Taifa* hutumika katika barua za kiofisi na machapisho ya serikali. Wanafunzi waliochagua kipotoshi E, *Fedha ya Tanzania* walichanganya dhana ya utajiri na fedha kama inavyotumika katika jamii na watu wengi, ambapo mtu mwenye fedha ndiye anayehesabika tajiri. Hivyo, walishindwa


kutenganisha fedha ya Tanzania na dhana nzima ya utajiri wa mali asili ya nchi yetu.

Kipengele cha (ii) kililenga kupima uwezo wa wanafunzi kutambua alama ya taifa inayotumiwa katika barua za kiofisi na machapisho ya serikali. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi D, *Nembo ya taifa* walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu alama ya taifa inayotumika kwenye barua za kiofisi na machapisho ya serikali. Walielewa vyema kuwa Nembo ya taifa ni ngao ya Taifa inayojumuisha mkuki, jembe na shoka pamoja na pembe mbili za ndovu, Bibi na Bwana, mlima Kilimanjaro na maandishi 'Uhuru na Umoja' ambayo hutumika katika nyaraka zote za serikali. Wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Bendera ya taifa,* walishindwa kutambua kuwa Bendera ya taifa huwakilisha uhuru wa nchi yetu. Vilevile, uwepo wa Bendera ya taifa kwenye Nembo ya taifa kulivutia wanafunzi kuchagua kipotoshi hicho. Aidha, wanafunzi wengine walichagua vipotoshi A, *Bendera ya taifa,* C, *Wimbo wa taifa*, E, *Fedha ya Tanzania* na F*, Pembe za ndovu* hawakuwa na uelewa sahihi kuhusu alama za taifa jambo lililowafanya washindwe kutofautisha alama moja na nyingine.

Kipengele cha (iii) kililenga kupima uwezo wa wanafunzi kutambua alama ya taifa inayoashiria uhuru wa nchi yetu. Wanafunzi walioweza kuchagua jibu sahihi A, *Bendera ya taifa* walitambua kuwa Bendera ya taifa mbali ya kuwa na rangi za kupendeza, pia huashiria uhuru wa nchi yetu. Wanafunzi waliochagua kipotoshi B, *Jembe na nyundo* hawakuwa na uelewa sahihi wa maana ya alama za taifa zinazopatikana kwenye nembo ya taifa. Hawakutambua kuwa jembe na nyundo huwakilisha vifaa vinavyotumika kuendeleza taifa. Wanafunzi wengine walivutiwa na kipotoshi C, *Wimbo wa taifa* kwa kuwa wimbo wa taifa huimbwa kila siku kabla ya masomo kuanza shuleni, ambapo ndani yake kuna beti inayohimiza kudumisha uhuru na amani. Wanafunzi waliochagua kipotoshi D, *Nembo ya taifa* hawakuelewa kuwa nembo ya taifa hutumika katika barua za kiofisi na machapisho ya serikali. Wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi E, *Fedha ya Tanzania* hawakuwa na ufahamu juu ya alama za taifa na maana zake, hivyo walichanganya uhuru wa nchi na uwepo wa Fedha ya Tanzania, hawakutambua kuwa fedha ni alama ya taifa ambayo hutumika kama njia ya kuuza na kununua bidhaa na huduma. Aidha, wanafunzi waliochagua kipotoshi F, *Pembe za ndovu* hawakuwa na uelewa wa kutosha kuwa *Pembe za ndovu* zinaashiria utajiri wa mali asili ya nchi yetu na si uhuru wa nchi yetu.

Kipengele cha (iv) kililenga kupima uwezo wa wanafunzi katika kubaini alama ya taifa ambayo huwakilisha vifaa vinavyotumika kuendeleza taifa. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi B, *Jembe na nyundo* walikuwa na uelewa sahihi ya kuwa *Jembe na nyundo* ni alama ya taifa inayotumiwa kuwakilisha vifaa vinavyotumika kuendeleza taifa. Walitambua kuwa *Jembe* katika taifa letu huwakilisha wakulima na *nyundo* huwakilisha wafanyakazi. Wanafunzi waliochagua vipotoshi A, *Bendera ya taifa*, C, *Wimbo wa taifa* na D, *Nembo ya taifa* hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu alama za Taifa letu. Wanafunzi waliochagua kipotoshi E, *Fedha ya Tanzania* walichanganya na dhana ya matumizi ya fedha katika kununua vifaa mbalimbali katika jamii wanamoishi kama vile redio, vyombo vya kupikia, vifaa vya shule, n.k. Aidha, wanafunzi waliochagua kipotoshi F, *Pembe za ndovu* walishindwa kutambua kuwa hii ni alama inayoonesha utajiri wa mali asili ya nchi yetu, hivyo si vifaa vinavyotumika kuendeleza taifa.

**Swali la 3:** Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu *Kuwa Mwadilifu.* Swali liliwataka wanafunzi kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi. Swali hili lilikuwa na vipengele vinne vilivyotoka katika umahiri mahususi mbalimbali na kila kipengele kilikuwa na alama 2. Kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili kulikuwa kwa wastani kwa kuwa ni asilimia 59.7 pekee ya wanafunzi ndio waliweza kupata alama 4 hadi 8. Wanafunzi 669,703 (40.3%) walishindwa kwa kupata alama 0 au 2. **Chati Na. 3** inaonesha takwimu za kufaulu kwa wanafunzi katika swali la 3.




**Chati Na. 3**: *Kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali la 3.*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kwa kuwa asilimia 59.7 ya wanafunzi walifaulu kwa kupata kuanzia alama 4 hadi 8.

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele.

(i) Kitendo cha mtoto kushiriki katika maamuzi huonyesha __________.

(wajibu wa mtoto, haki ya mtoto, kukomaa kwa mtoto)

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi *Kusimamia haki* na kililenga kupima ufahamu wa mwanafunzi kuhusu dhana na matendo yanayoonesha haki katika jamii na familia. Wanafunzi walioweza kuchagua na kuandika jibu sahihi *haki ya mtoto* walidhihirisha uelewa wa kutosha juu ya matendo ya haki za watoto yanayofanyika katika jamii na familia, kama vile kushiriki katika maamuzi, kupewa elimu, kupewa vitu muhimu kama chakula, nguo na malazi, n.k.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliokosa kipengele hiki walivutiwa na vipotoshi *wajibu wa mtoto* na *kukomaa kwa mtoto*. Wanafunzi hao hawakuwa na uelewa juu ya maana sahihi ya haki na wajibu wa mtoto katika familia na jamii kwa ujumla. Walishindwa kutambua kuwa *wajibu* ni mambo ambayo mtu anapaswa kuyatimiza kama vile kuwatii na kuwaheshimu wengine, kusaidia kazi ndogondogo za nyumbani, n.k.

Wanafunzi waliochagua *kukomaa kwa mtoto* walichanganya na tabia za wazazi kupongeza watoto wao wanaposhiriki katika shughuli mbalimbali za familia kwa kuonesha ukomavu na ushujaa lakini walishindwa kutambua kuwa hayo si matendo ya haki za mtoto. Wanafunzi wengine waliandika majibu mengine ambayo hayakuwa katika chaguzi zilizotolewa. Hivyo kukosa kipengele hiki. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alindika *kushiriki na watu wengine* na kati yao walikuwepo walioacha wazi bila kujaza jibu lolote.

(ii) Ili watoto wapate msaada mara wanapohitaji wanatakiwa wawe ____________________.(wanafiki, wakweli, wazembe)

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi *Kuaminika katika jamii* na kililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kubaini matendo yanayojenga tabia ya uaminifu katika maisha ya kila siku. Wanafunzi waliochagua na kuandika jibu sahihi *wakweli* walikuwa na ufahamu kuwa, ili watoto katika jamii wapate msaada mara wanapohitaji wanatakiwa wawe wakweli. Wanafunzi hao walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu matendo yanayojenga uaminifu katika jamii, kama vile kuwa mkweli, muaminifu na kuepuka kuwa msaliti.

Wanafunzi waliokosa kipengele hiki walichagua vipotoshi *wanafiki* na *wazembe*. Wanafunzi waliochagua na kuandika kipotoshi *wanafiki* hawakuwa na uelewa juu ya maana sahihi ya dhana hiyo kwa kuwa mnafiki hawezi kupata msaada mara anapouhitaji kwa kuwa hiyo ni tabia mbaya mbele ya jamii. Hawakujua kuwa mnafiki ni mtu anayefanya mambo kinyume na anavyosema au anavyoahidi. Wanafunzi waliochagua na kuandika *wazembe* walidhani mtoto anapokuwa mzembe ni rahisi kupata msaada mara anapouhitaji lakini walishindwa kutambua kuwa uzembe ni kitendo kibaya. Wanafunzi wachache walinakili majibu yote kwenye mabano na kuyajaza katika nafasi ya wazi, hivyo kukosa alama za kipengele hiki.

(iii) Lipi kati ya yafuatayo ni wajibu wa mtoto? ________________________.

(Kupendwa, kupata chakula, kufanya kazi rahisi)

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi *Kusimamia haki* na kililenga kupima uwezo wa wanafunzi katika kubaini matendo ya wajibu wa mtoto

yanayotendwa katika familia na jamii. Uchambuzi uliofanywa kwenye skripti za wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi wengi waliweza kupata jibu sahihi *kufanya kazi rahisi.* Wanafunzi hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu wajibu wa watoto katika familia na jamii nzima. Walibaini kuwa watoto wana wajibu wa kushiriki katika shughuli mbalimbali za familia na jamii kwa kufanya kazi rahisi kama kufagia uwanja, kuosha vyombo, kupanda maua, n.k.

Kwa upande mwengine, wanafunzi walioshindwa kipengele hiki walichagua vipotoshi *kupendwa* na *kupata chakula*. Wanafunzi hao hawakuweza kutofautisha matendo ya wajibu na haki. Hawakuelewa kuwa haki ni kitu muhimu ambacho mtu anapaswa kupewa, kama vile kuishi, kupendwa, kupata chakula, kupata elimu na malezi bora. Kwa hiyo, *kupendwa* na *kupata chakula* ni haki ya kila mtoto. Walishindwa kutambua kuwa wajibu ni majukumu ambayo mtu anapaswa kuyatimiza.

(iv) Kitendo cha mtu kufanya kazi aliyopangiwa huitwa ______________.

(wajibu, haki, uaminifu)

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi *Kusimamia haki* na kililenga kupima uelewa wa mwanafunzi kubaini matendo ya wajibu. Wanafunzi wengi waliochagua kipotoshi *haki* na *uaminifu* hawakuwa na maarifa juu ya dhana nzima ya haki na uaminifu. Walishindwa kutambua kuwa haki ni mambo muhimu anayopaswa kupewa mtu kama kupendwa, kupewa chakula, kupewa elimu, n.k. Wanafunzi hao hawakuwa na uelewa kuwa uaminifu ni hali ya kukubalika au kuaminika kwa watu kiasi cha wao kukupatia dhamana ya mamlaka fulani na si kufanya kazi uliyopangiwa.

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi *wajibu* walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana sahihi ya neno wajibu. Walitambua kuwa kitendo cha mtu kufanya kazi aliyopangiwa ni wajibu, ambapo kazi hizo huweza kuwa za shuleni au nyumbani, kama vile kushiriki katika usafi wa mtaa, kuosha vyombo, kukamilisha zoezi darasani, n.k. **Kielelezo Na. 3.1** ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika majibu sahihi katika swali hili.

3. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(i) Kitendo cha mtoto kushiriki katika maamuzi huonyesha haki ya mtoto.
(wajibu wa mtoto, haki ya mtoto, kukomaa kwa mtoto)

(ii) Ili watoto wapate msaada mara wanapohitaji wanatakiwa wawe wakweli.
(wanafiki, wakweli, wazembe)

(iii) Lipi kati ya yafuatayo ni wajibu wa mtoto? kufanya kazi rahisi.
(kupendwa, kupata chakula, kufanya kazi rahisi)

(iv) Kitendo cha mtu kufanya kazi aliyopangiwa huitwa wajibu.
(wajibu, haki, uaminifu)

**Kielelezo Na. 3.1**: Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi.

Katika Kielelezo Na. 3.1 mwanafunzi alielewa vema matakwa ya swali na aliweza kuchagua na kuandika majibu sahihi kwa vipengele vyote vinne, hivyo alipata alama zote 8 za swali hili.

Hata hivyo, wapo wanafunzi walioshindwa kuchagua na kuandika majibu sahihi kama ilivyochambuliwa katika kipengele (i) – (iv). **Kielelezo Na. 3.2** kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa swali hili.

3. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(i) Kitendo cha mtoto kushiriki katika maamuzi huonyesha

Wajibuwamtoto

(wajibu wa mtoto, haki ya mtoto, kukomaa kwa mtoto)

(ii) Ili watoto wapate msaada mara wanapohitaji wanatakiwa wawe

Wanafiki .

(wanafiki, wakweli, wazembe)

(iii) Lipi kati ya yafuatayo ni wajibu wa mtoto?

kupata chakula .

(kupendwa, kupata chakula, kufanya kazi rahisi)

(iv) Kitendo cha mtu kufanya kazi aliyopangiwa huitwa uaminifu .

(wajibu, haki, uaminifu)

**Kielelezo Na. 3.2**: Sampuli ya majibu yasiyosahihi ya mwanafunzi.

Katika Kielelezo Na. 3.2 mwanafunzi alichagua na kuandika majibu yasiyo sahihi hali inayoashiria mwanafunzi hakuwa anajua matendo ya kusimamia haki na kuaminika katika jamii.


## 2.2 Sehemu B (Alama 24)

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3) swali la 4, 5, na la 6. Swali la 4 lilimtaka mwanafunzi kuonesha zana za asili au siyo za asili kwa kuweka alama ya vema (√ ) kwenye sehemu inayohusika. Swali la 5 lilikuwa la kuchunguza picha, kisha kujibu maswali yanayofuata na swali la 6 lilikuwa la kusoma kifungu cha habari, kisha kujibu kipengele (i) – (iv) katika sehemu zilizoachwa wazi. Kila swali katika sehemu hii lilikuwa na alama 8. Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika sehemu hii.

**Swali la 4:** Jibu vipengele (i) – (v) kwa kuweka alama ya **vema** (√) kuonyesha kama zana zilizowekwa kwenye jedwali ni za asili au siyo za asili. Namba moja imetolewa **kama mfano**.

| Na. | Zana | Zana za Asili | Zana Zisizo za Asili |
|---|---|---|---|
| (i) | Gitaa | | √ |
| (ii) | Manyanga | | |
| (iii) | Kinanda | | |
| (iv) | Filimbi | | |
| (v) | Tarumbeta | | |

Swali lilikuwa na vipengele vinne, (ii) (iii), (iv) na (v), vilivyotoka katika umahiri mkuu *Kudumisha Amani* kwenye umahiri mahususi *Kuheshimu tofauti za kiutamaduni na mitazamo ya watu wa jamii tofauti.* Swali lilimtaka mwanafunzi kubaini zana mbalimbali za asili na zisizo za asili zinazotumika katika jamii zetu. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani asilimia 14.7 ya wanafunzi 1,663,778 walipata alama 8, asilimia15.8 walipata alama 6, asilimia 29.3 walipata alama 4 na asilimia 40.2 walipata alama 0 au 2. **Chati Na. 4** inaonesha takwimu za kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili.




**Chati Na 4:** *Kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali la 4.*

Chati Na. 4 inaonesha kuwa kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili kulikuwa kwa kiwango cha wastani. Hii ni kwa kuwa asilimia 59.8 ya wanafunzi wote waliofanya swali hili walipata daraja A hadi D.

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele:

Kipengele (ii) kiliwataka wanafunzi kuonesha kama manyanga ni zana ya asili au siyo ya asili. Wanafunzi waliokuwa na uelewa wa kutosha wa zana za asili zinazopatikana katika jamii zetu waliweza kubaini jibu sahihi kuwa manyanga ni zana ya asili. Wanafunzi hao walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha juu ya ala za asili mbalimbali zinazotumika katika muziki na ngoma za makabila tofauti kama mdundiko, sindimba, n.k.

Wanafunzi walioshindwa kubaini kuwa manyanga ni zana ya asili hawakuwa na uelewa kuhusu Manyanga. Hawakujua kuwa manyanga ni ala ya muziki ambapo mbegu, gololi au mawe hutiwa ndani ya chombo kama kibuyu au kopo au chupa ambayo hutoa sauti inapotikiswa.

Kipengele (iii) kiliwataka wanafunzi kuonesha kama kinanda ni zana ya asili au siyo ya asili. Wanafunzi waliokuwa na ufahamu wa kutosha wa zana zisizo za asili waliweza kubaini jibu sahihi kuwa kinanda siyo zana ya asili. Walitambua kuwa kinanda ni chombo cha muziki kinachotoa sauti mbalimbali za nyimbo kinapobofywa vitufe vyake.

Wanafunzi waliobainisha kuwa kinanda ni zana ya asili walidhihirisha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuweza kutofautisha zana za asili na zisizo za asili. Walishindwa kutambua kuwa chimbuko la kinanda ni kutoka katika utamaduni wa muziki wa nchi za magharibi.

Kipengele (iv) kiliwataka wanafunzi kubainisha kama filimbi ni zana ya asili au siyo ya asili. Wanafunzi waliochagua ni zana ya *asili* walitambua kuwa filimbi ni miongoni mwa zana za asili ambayo hutumika kwenye ngoma za jadi. Aidha, baadhi ya wanafunzi walitumia uzoefu wao wa maisha ya kila siku na kupitia njia za mawasiliano kama televisheni ambapo ngoma za asili za makabila mbalimbali huoneshwa na filimbi ikiwa mojawapo ya zana inayotumiwa na vikundi vya ngoma za asili.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua kuwa ni zana isiyo ya asili walionesha kukosa uelewa wa kutosha juu ya zana za asili. Wanafunzi hao walishindwa kutofautisha kati ya filimbi inayotumika katika ngoma za jadi na zile zinazotumika katika mchezo wa mpira wa miguu au katika shughuli za ulinzi. Hii inatokana na kuwa wanafunzi wengi wamezoea kuona refa wa mpira akitumia filimbi kutoa maelekezo mbalimbali uwanjani, vilevile mgambo wanatumia filimbi wakati wanakimbiza wahalifu. Hivyo, kuwapelekea wanafunzi hawa kudhani kuwa filimbi haiwezi kuwa zana ya asili.

Kipengele (v) kiliwataka wanafunzi kubaini kama tarumbeta ni zana ya asili au siyo ya asili. Wanafunzi waliokuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu zana zisizo za asili waliweza kubaini jibu sahihi kuwa tarumbeta ni zana isiyo ya asili. Walikuwa na uelewa kuwa tarumbeta ni ala ya muziki iliyotengenezwa na shaba na ambayo hutoa sauti mbalimbali kwa kupuliza na kubonyeza vali zake. Walielewa kuwa asili yake ni katika utamaduni wa muziki wa nchi za kimagharibi, hususani katika muziki wa “jazz”.

Wanafunzi waliochagua zana za asili walikuwa hawana uelewa wa kutosha juu ya zana zisizo za asili. Wanafunzi hao, hasa wale wa mijini wamezoea kuona tarumbeta ikipigwa wakati wa sherehe mitaani na majumbani, hivyo kudhani kwamba tarumbeta ni zana ya asili.

**Swali la 5:** Swali hili liliwataka wanafunzi kuchunguza kwa makini picha ifuatayo kisha kujibu maswali yanayofuata.



**Maswali**


(i) Ni kitendo gani kinaoneshwa katika picha? ____________________ .

(ii) Unafikiri kwanini mtu huyu katika picha anafanya kitendo hiki? ______________________________ .

(iii) Ni hasara gani inayosababishwa na kitendo kinachofanyika katika picha? ________________________ .

(iv) Pendekeza njia mojawapo inayoweza kutumika kulinda na kutunza mazingira ya eneo liliooneshwa kwenye picha ________________ .

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu, *Kuithamini Jamii*, na kwenye umahiri mahususi, *Kutunza mazingira na vilivyomo*. Swali lililenga kupima ufahamu wa wanafunzi kuhusu madhara yanayotokana na ukataji miti ovyo. Swali hili lilikuwa na vipengele vinne na kila kimoja kilikuwa na alama 2. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani; asilimia14.0 ya wanafunzi 1,663,778 walipata alama 8, asilimia 20.6 walipata alama 6, asilimia 22.9 alama 4 na asilimia 42.5 walipata alama 0 au 2 kama inavyoonekana katika **Chati Na. 5**.




**Chati Na 5 :** *Kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali la 5.*

Chati Na. 5 inaonesha kuwa kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kwa kuwa asilimia 57.5 ya wanafunzi walifaulu kwa kupata kuanzia alama 4 hadi 8.

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele:

(i) Ni kitendo gani kinaoneshwa katika picha? ________________ .

Kipengele hiki kililenga kupima ufahamu wa wanafunzi kuhusu matendo ya uharibifu wa mazingira, kama vile ukataji miti ovyo. Wanafunzi waliojibu *ukataji wa miti/uharibifu wa mazingira* walikuwa na ufahamu na maarifa ya kutosha juu ya matendo ya ukataji ovyo wa miti. Walitambua kuwa mazingira ni kila kitu kinachotuzunguka kama hewa, wanyama, ardhi na mimea, hivyo ni jukumu letu kuitunza. Kwa hiyo, kitendo cha kukata miti ovyo ni miongoni mwa matendo ya uharibifu wa mazingira.

Kwa upande mwingine, wanafunzi ambao walipata alama 0 katika kipengele hiki, baadhi yao walishindwa kubaini matakwa ya swali, hivyo kutoa majibu ambayo hayaendani na kitendo kinachoonekana katika mchoro, kama vile *panga, haki, mifugo mbuzi na ng'ombe, barabara, miti*, n.k. Aidha, wengine walikosa stadi za KKK, hivyo kuandika majibu yasiyoeleweka.

(ii) Unafikiri kwa nini mtu huyu katika picha anafanya kitendo hiki?

______________________.

Kipengele hiki kiliwataka wanafunzi kubaini sababu zinazosababisha watu kukata miti ovyo. Wanafunzi waliotaja sababu zifuatazo *uhitaji wa kuni, mkaa, mbao, kuanzisha mashamba na makazi mapya* walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya sababu mbalimbali zinazopelekea watu kujihusiha na ukataji miti ovyo. Wanafunzi hao walitambua kuwa chanzo kikuu cha nishati kwa wananchi walio wengi ni kuni na mkaa. Hali hii huchangia kasi kubwa ya ukataji wa miti ovyo. Pia, kuna mahitaji makubwa ya mbao katika shughuli za ujenzi na viwanda vya samani. Kwa upande mwingine, kilimo cha wananchi walio wengi siyo cha kisasa. Hali hii husababisha kuhama mara kwa mara na kukata miti kuanzisha mashamba mapya.

Kwa upande mwingine, wanafunzi ambao walishindwa kubaini matakwa ya swali waliandika hoja mbalimbali zisizo sahihi kama vile *utunzaji wa rasilimali, ili kupata pesa*, *anasafisha mazingira*, *miti inaleta mbu, ana maisha magumu,* n.k., majibu ambayo yalisababisha wapate ufaulu hafifu katika kipengele hiki.

(iii) Ni hasara gani inayosababishwa na kitendo kinachofanyika katika picha? ______________________________ .

Kipengele hiki kilipima ufahamu wa wanafunzi kuhusu madhara yatokanayo na ukataji miti ovyo. Baadhi ya wanafunzi walioshindwa kipengele hiki hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu madhara ya uharibifu wa mazingira, hivyo kuwasababisha kuandika majibu ambayo hayakuwa sahihi, kama vile *kukata miti ovyo, ni kitendo kibaya, kuugua malaria, n.k.* Aidha, wanafunzi wengine walikosa stadi za KKK, hivyo kuandika maneno yasiyoeleweka au kuacha sehemu hiyo bila kujibu chochote.

Kwa upande mwengine, wanafunzi waliobaini matakwa ya swali walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya madhara yatokanayo na ukataji ovyo wa miti na waliweza kutaja sababu mbalimbali, kama vile *ukosefu wa mvua/ukame*, *mmomonyoko wa udongo/jangwa/ kupotea kwa viumbe hai na ukosefu wa*

*hewa safi*. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa kuwa miti inapaswa kutunzwa kwani katika maisha ya kila siku hewa itokayo katika miti inahitajika. Pia inahitajika ardhi nzuri yenye rutuba kwa ajili ya kilimo.

(iv) Pendekeza njia mojawapo inayoweza kutumika kulinda na kutunza mazingira ya eneo liliooneshwa kwenye picha.

________________________________________ .

Kipengele hiki kiliwataka wanafunzi kubaini njia zinazoweza kutumika kutunza mazingira yaliyoooneshwa katika picha. Wanafunzi waliokuwa na ufahamu na maarifa ya kutosha juu ya njia zinazoweza kutumiwa kutunza mazingira waliweza kuandika jibu sahihi *kupanda miti/kuzuia ukataji wa miti* na *matumizi ya nishati mbadala.* Aidha, baadhi ya wanafunzi walitumia uzoefu wao wa maisha yao ya kila siku kutoa mapendekezo ya namna bora ya kutunza mazingira kwani swala la mazingira ni mtambuka. Kupitia vyombo mbalimbali vya mawasiliano elimu juu ya utunzaji wa mazingira inatolewa katika jamii na kuwafikia watu wengi wakiwemo wanafunzi. Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri.

**Maswali**

(i) Ni kitendo gani kinaoneshwa katika picha? ukataji miti ovyo.

(ii) Unafikiri kwanini mtu huyu katika picha anafanya kitendo hiki? ili kupata mbao za kuuza, kuni na kuchoma mkaa

(iii) Ni hasara gani inayosababishwa na kitendo kinachofanywa katika picha? kusababisha jangwa na mmomonyoko wa udongo

(iv) Pendekeza njia mojawapo inayoweza kutumika kulinda na kutunza mazingira ya eneo lililooneshwa kwenye picha kupanda miti kwa wingi na kutokata miti ovyo.

**Kielelezo Na. 5.1** ni sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi.


Katika Kielelezo Na. 5.1, mwanafunzi aliweza kuchunguza picha vizuri na hivyo aliweza kuandika majibu sahihi kwa vipengele vyote vinne na kupata ufaulu mzuri.

**Swali la 6:** Swali hili liiwataka wanafunzi kusoma kwa makini kifungu cha habari, kisha kujibu maswali.

*Vyanzo vya maji ni muhimu katika maisha yetu. Mfano wa vyanzo vya maji ni mito, maziwa, bahari, mabwawa, visima, mvua na chemichemi. Tunapaswa kuvilinda vyanzo hivi vya maji. Tunaweza kuvilinda vyanzo vya maji kwa kutokata miti ovyo kandokando ya vyanzo vya maji, kupanda miti, kutojisaidia au kutupa taka kwenye vyanzo vya maji.*

*Maji yanatumika kwa kunywa, kupikia, kuoshea, kuoga, kusafisha na kumwagilia mazao. Ni wajibu wa jamii nzima kuvilinda vyanzo vya maji.*

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu, *Kuithamini Jamii,* kwenye umahiri mahususi, *Kutunza mazingira na vilivyomo*. Swali hili lilikuwa na vipengele vinne na kila kipengele kilikuwa na alama 2. Swali hili lililenga kupima ufahamu wa wanafunzi kuhusu vyanzo mbalimbali vya maji, matumizi ya maji na jinsi ya kutunza vyanzo hivyo. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani. Asilimia 30.4 ya wanafunzi 1,663,778 walikuwa na alama 8; asilimia19.70 walikuwa na alama 6; asilimia 16.2 walikuwa na alama 4; wakati asilimia 33.7 walikuwa na alama 0 au 2. Kwa ujumla, kiwango hiki cha kufaulu ni cha wastani kwa kuwa asilimia 66.3 ya wanafunzi waliofanya swali hili walifaulu kwa kupata kati ya kiwango cha wastani hadi kiwango kizuri sana kama inavyoonekana katika **Chati Na. 6**.




**Chati Na. 6:** *Kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali la 6.*

Chati Na. 6 inaonesha kuwa, wanafunzi walikuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu katika swali hili kwa kuwa asilimia 66.3 ya wanafunzi walipata kuanzia alama 4 hadi 10.

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele:

(i) Kulingana na kifungu hiki cha habari, mito, maziwa, bahari, mabwawa na mvua huitwa ______________________________ .

Kipengele hiki kiliwataka wanafunzi kutaja jina la jumla la mito, maziwa, bahari, mabwawa na mvua kama lilivyoainishwa kwenye habari hii. Kipengele hiki kililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu vyanzo vya maji. Wanafunzi walioweza kusoma na kukielewa vema kifungu cha habari waliandika jibu sahihi *vyanzo vya maji.* Wanafunzi hao waliweza kuhawilisha maarifa kwani vyanzo hivi vingi vya maji hupatikana kwenye mazingira wanayoishi.

Kwa upande mwingine, wanafunzi walioshindwa kuelewa kifungu cha habari walitoa majibu ambayo si sahihi, kama vile *chemichemi, mawingu, maji, masika, mabwawa, n.k.* Kwa ujumla, wanafunzi hao walikosa msamiati ambao ungesimama badala ya mito, maziwa, bahari, mabwawa na mvua.

(ii) Ni nani anawajibika kulinda vyanzo vya maji? ________________ .

Kipengele hiki kiliwataka wanafunzi kubaini anayewajibika kulinda vyanzo vya maji katika jamii zetu. Wanafunzi waliosoma na kukielewa vema kifungu cha habari, waliweza kuandika jibu sahihi *jamii nzima*. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa kuwa maji ni rasilimali muhimu, hivyo ni vizuri rasilimali hii ikatumika kwa uangalifu na kutunzwa na jamii nzima.

Aidha, wanafunzi walioshindwa kuandika jibu sahihi walishindwa kuelewa kifungu cha habari walichopewa, hivyo kuandika majibu yasiyo sahihi, kama vile *mgambo, polisi, mwenyekiti wa kijiji na wazazi kupanda miti kwa wingi zaidi, aliyeteuliwa,* n.k. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa jamii nzima ina jukumu la kutunza vyanzo vya maji. Wengi walivutiwa na mazingira halisi wanayotoka kwani baadhi ya jamii, hasa wale wanaotoka katika mazingira yenye uhaba wa maji. Viongozi wao wa kijiji husimamia ugawaji wa maji ya mabomba au visima na kuweka ulinzi maalumu.

(iii) Tunawezaje kuvitunza vyanzo vya maji? ______________________ .

Kipengele hiki kiliwataka wanafunzi kutaja njia zinazoweza kutumika kutunza vyanzo vya maji. Wanafunzi waliosoma na kuelewa kifungu cha habari waliandika jibu sahihi *kutokata miti ovyo/kupanda miti/ kutojisaidia kwenye vyanzo vya maji/kutotupa taka kwenye vyanzo vya maji.* Wanafunzi hao walionesha uelewa wa kutosha kuhusu njia zilizoainishwa katika habari za kulinda vyanzo vya maji.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi hawakuelewa kifungu cha habari, hivyo waliandika majibu mbalimbali ambayo hayakuwa sahihi, kama vile *kuweka walinzi, kufanyia usafi mara kwa mara vinapochafuka*, n.k. Aidha, baadhi ya wanafunzi walikosa stadi za KKK, hivyo kuandika majibu yasiyoeleweka.

(iv) Tunatumia maji kwa shughuli zipi? ______________________ .

Kipengele hiki kiliwataka wanafunzi kutaja matumizi ya maji na kililenga kupima ufahamu wa wanafunzi juu ya matumizi ya maji. Kipengele hiki kilijibiwa kwa usahihi na wanafunzi wengi kwa sababu maji ni rasilimali muhimu ambayo wanaitumia katika shughuli zao za kila siku, hivyo iliwawia rahisi kutaja matumizi ya maji. Vilevile, wanafunzi hao walidhihirisha kuwa na uwezo wa kusoma na kuelewa vema kifungu cha habari kilichotolewa. Baadhi ya hoja sahihi zilizotolewa na wanafunzi hao ni kama vile *kunywa, kupikia, kuoshea, kuoga, kusafisha na kumwagilia mazao.* **Kielelezo Na. 6** ni sampuli ya majibu mazuri ya mwanafunzi katika swali hili.

**Maswali**

(i) Kulingana na kifungu hiki cha habari, mito, maziwa, bahari, mabwawa na mvua huitwa vyanzo vya maji.

(ii) Ni nani anawajibika kulinda vyanzo vya maji? kila mtu na jamii nzima inapaswa kulinda vyanzo vya maji

(iii) Tunawezaje kuvitunza vyanzo vya maji? kupanda miti kandokando ya vyanzo vya maji na kutojisaidia kwenye maji.

(iv) Tunatumia maji kwa shughuli zipi? kuogea, kupikia na kufulia.

**Kielelezo Na. 6** Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi.

Katika kielelezo Na. 6 mwanafunzi alielewa vema matakwa ya kila kipengele, hivyo kutoa majibu sahihi kwa vipengele vyote vinne.

Kwa upande mwingine, wanafunzi wachache hawakuelewa kifungu cha habari, hususan kwenye matumizi ya maji katika maisha ya kila siku, hivyo kutoa majibu ambayo si sahihi, kama vile *tunaweza kuvilinda vyanzo vya maji,* n.k. Kati yao, wengine hawakuwa na stadi za KKK, hivyo kushindwa kusoma na kuandika majibu yanayosomeka.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI

Uchambuzi wa umahiri katika maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Uraia na Maadili unaonesha kuwa, baadhi ya umahiri ulikuwa na ufaulu mzuri na mwingine ulikuwa na ufaulu wa wastani. Kwa ujumla, ufaulu kwa wanafunzi katika umahiri wote ulikuwa wa wastani. Aidha, umahiri wa *Kuwa Mstahimilivu* katika swali la 1 ulikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu cha asilimia 79.6. Umahiri wote uliobakia katika upimaji huu ulikuwa na ufaulu wa kiwango cha wastani ambapo umahiri wa *Kuithamini Jamii* katika swali la 5 na 6 (61.9%), *Kudumisha Amani* katika swali la 4 (59.8%), Kuwa Mwadilifu katika swali la 3 (59.7%) na Kuwa Mwajibikaji katika swali la 2, ulikuwa na ufaulu wa asilimia 44. Taarifa zaidi za kufaulu kwa wanafunzi katika kila umahiri zimeoneshwa katika Kiambatisho A na B.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika maswali ya upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Uraia na Maadili unaonesha kuwa, kwa ujumla, wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri ambapo asilimia 95.26 ya wanafunzi walipata kiwango cha wastani hadi kizuri sana cha daraja A hadi daraja D na wanafunzi wachache (4.74%) walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata daraja E. Umahiri wote ulipimwa ambao ni *Kuthamini Jamii*, *Kuwa Mwajibikaji*, *Kuwa Mwadilifu*, *Kuwa Mstahimilivu* na *Kudumisha Amani* ambapo kati ya huo, umahiri wa *Kuwa Mstahimilivu* ulikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu. Umahiri uliobaki ulikuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu. Wanafunzi waliofanya vizuri katika Upimaji huu walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika umahiri uliopimwa, uelewa mzuri wa maswali mbalimbali yaliyoulizwa na kuwa na stadi za ufahamu. Vilevile, wanafunzi hao walimudu vyema stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK).

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, zipo changamoto mbalimbali za wanafunzi wachache walioshindwa kupata alama za juu kama; kutokuwa na maarifa ya kutosha katika umahiri uliopimwa, kukosa stadi za KKK na hivyo kushindwa kuandika sentensi zinazoeleweka na kushindwa kujua mahitaji ya swali. Pia walionesha kukosa stadi za ufahamu na hivyo kushindwa kujibu swali la ufahamu kwa usahihi.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi, Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza mambo yafuatayo:

(a) Walimu waongeze juhudi katika kufundisha umahiri wote ulioainishwa katika muhtasari. Watakiwe kuhakikisha wanafunzi wanakuwa mahiri kwa kuwapima kwa kiwango cha juu cha utendaji hasa katika umahiri uliokuwa na kiwango cha kufaulu cha wastani ambao ni *Kuithamini Jamii*, *Kudumisha Amani*, *Kuwa Mwadilifu* na *Kuwa Mwajibikaji*.

(b) Walimu wa Darasa la I na II watakiwe kuweka mikakati maalumu kwa kutumia vitabu na mbinu mbalimbali za kufundishia kuhakikisha wanafunzi wanaofanya Upimaji wa Darasa la Nne wanakuwa na stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK).

(c) Wanafunzi wanatakiwa kuhamasishwa na kuongozwa katika kusoma vitabu vya kiada na rejea ili kuongeza uelewa wao katika umahiri mbalimbali wa somo hili.

(d) Walimu waandae majaribio na mitihani inayokuza uwezo wa wanafunzi kujibu maswali yanayopima stadi mbalimbali (Kuandika, Kusoma na Kuhesabu).

***Kiambatisho A***

## UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI

**06 Uraia na Maadili**

| Na | Umahiri | UPIMAJI WA 2019 | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kufaulu kwa kila swali | | Wastani wa kufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya Swali | % za kufaulu | | |
| 1 | Kuwa Mstahimilivu | 1 | 79.6 | 79.6 | Nzuri |
| 2 | Kuithamini Jamii | 5 | 57.5 | 61.9 | Wastani |
| | | 6 | 66.3 | | |
| 3 | Kudumisha Amani | 4 | 59.8 | 59.8 | Wastani |
| 4 | Kuwa Mwadilifu | 3 | 59.7 | 59.7 | Wastani |
| 5 | Kuwa Mwajibikaji | 2 | 44 | 44 | Wastani |

*Kiambatisho B*

## MUHTASARI WA KUFAULU KWA WANAFUNZI KWA KILA UMAHIRI KATIKA SFNA 2019 SOMO LA URAIA NA MAADILI

